# Ubia Mkakati wa Mnyororo wa Thamani kwenye Zao la Alizeti

SAGCOT
SOUTHERN AGRICULTURAL GROWTH CORRIDOR OF TANZANIA

## Muhtasari


Alizeti (Helianthus annuus) ni moja ya minyororo ya thamani ya vipaumbele ndani ya kongani ya Mbarali katika Ukanda wa SAGCOT. Mnyororo wa thamani kwenye alizeti una uwezo wa kuchangia kwa kiwango kikubwa katika kuongeza kipato cha wakulima wadogo na kutengeneza fursa za ajira kwa vijana na kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi wa Tanzania. Kwa kuzingatia kuwa kuna mahitaji makubwa ya mafuta ya alizeti kwenye soko la ndani na je ya nchi, Kituo cha SAGCOT kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine wamechukua hatua mbalimbali kusaidia ukuaji wa mnyororo wa thamani kwenye alizeti ambayo ni mojawapo ya minyororo ya thamani iliyopewa vipaumbele kwenye Awamu ya Pili ya Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Killimo (ASDP II). Baadhi ya jitihada zilizochukuliwa ni motisha ya kikodi, na utambulishaji wa mbegu bora za alizeti ili kukuza tija kwenye uzalishaji wa mafuta ya alizeti.

Mpango wa SAGCOT unatekelezwa kuzingatia sera na mipango ya serikali kama Mpango wa Kundeleza Sekta ya Kilimo (ASDP). Kwa hivyo basi, alizeti imepewa kipaumbele kama mojawapo ya minyororo ya thamani ndani ya mpango wa SAGCOT. Kituo cha SAGCOT (SCL) kimeitisha mikutano kadhaa na Ubia Mkakati wa Alizeti kushughulikia masuala muhimu ya kisera na yasiyo ya kisera ili kuongeza ukuaji wa mnyororo wa thamani wa alizeti. Kituo cha SAGCOT kimeendelea kushiriki katika mikutano mbalimbali ya kisera ili kufanikisha maboresho ya kisera na kuhakikisha kuna mazingira mazuri yatakayochangia maendeleo ya mnyororo wa thamani wa zao la alizeti




## Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT)

Mpango wa SAGCOT ni ubia kati ya sekta ya umma na binafsi unaolenga kuchochea Uwekezaji kwenye Kilimo biashara katika ukanda wa kusini mwa Tanzania. Kituo cha SAGCOT kinafanya kazi kama dalali wa ubia na kitovu cha habari kwa wabia wa SAGCOT katika kuwezesha uwekezaji kwenye minyororo ya thamani inayoshirikisha jamii na kuzingatia uhifadhi endelevu wa mazingira. Kila mwaka, aina mbalimbali za ubia mkakati zimeibuka ambazo Mpango wa SAGCOT unashiriki kikamilifu kukuza na kuwezesha kutokana na Matukio makuu na yanayoweza kupanua shughuli hizi

## Nini kinasabisha ubia wa alizeti kuwa ubia mkakati?

Tanzania huagiza toka nje ya nchi asilimia (60%) ya mafuta ya kupikia chakula yanayogharimu zaidi ya dola la kimarekani milioni 250 kwa mwaka. Hata hivyo, sekta ya alizeti imeanza kuonyesha mabadiliko kutokana na uamuzi wa serikali kutoa motisha ya kikodi jambo ambalo limehimiza uwekezaji wa ndani ya nchi kwenye viwanda vya sekta ya mafuta ya alizeti, vilevile kutoa upendeleo katika mabadiliko ya tozo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa ndani wa mafuta ya alizeti. Maboresho kwenye sekta ya kodi na biashara ya mwaka wa fedha 2017/18 yameondoa kodi ya onegezeko la thamani (VAT) kwenye vifaa vya kuchakata mazao ya kilimo ikijumuisha vifaa/mashine za kukamua na kusafisha mafuta ghafi ya kula ambapo imelazimu uzalishaji wa mafuta ya alizeti wenye bei shindanishi sokoni. Wakati huohuo, kuondolewa kwa tozo ya kodi ya VAT kwenye mashudu ya alizeti kumeimarisha uchuni wa wachakataji/wasindikaji wa mafuta ya alizeti huku uamuzi wa kutoza asilimia (10%) kwenye mafuta ghafi na asilimia (25%) kwenye mafuta yaliyosafishwa yatokayo nje ya nchi yanayoleta ushindani kwa mafuta yanayozalishwa nchini kumepunguza hali ya ushindani kwenye soko la hapa ndani. Mabadiliko ya kodi na tozo yamebadili taswira ya sekta nzima kwa kuwahimiza wawekezaji kupata mbegu chotara, uchakataji/usindikaji na uwekezaji mwingine katika sekta ya alizeti. Sekta ya mbegu imekuwa ya kwanza kuitikia kwa kununua mbegu chotara toka nje ya nchi na kwa sasa uzalishaji wa mbegu hizi umeshaanza rasmi hapa nchini.

- **Uwezo wa kubadili hali ya mkulima kutoka mkulima mdogo hadi kuwa mkulima biashara na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza umaskini:** Mahitaji makubwa ya mafuta ya alizeti ya kula kama alizeti kwenye soko la ndani, kikanda na kimataifa inawezesha kubadili hali za wakulima wadogo kuwa wakulima biashara. Pia, kwa kuchakata/kusindika mafuta ya alizeti kunaweza kwa kiasi kikubwa kutengeneza ajira na hatimaye kupunguza umaskini.
- **Kutafuta masuluhisho ya kudumu katika mnyororo wa thamani:** ili kuhakikisha mnyororo wa thamani unakua kuna umuhimu mkubwa kwa wadau ndani ya mnyororo wa thamani kufanya kazi kwa kushirikiana katika kutafuta suluhisho la changamoto za kisekta kwa pamoja.

- **Ubia wa Alizeti ni kama uwanja wa kutoa mrejesho kwa watunga sera:** Ubia Mkakati wa Alizeti unatoa wasaa na nafasi ya kutoa mrejesho kwa watunga sera na kuwapa muda wa kupitia sera hizo kulingana na kipindi cha muda wanapotakiwa kufanya hivyo.
- **Kuonyesha athari chanya za kimazingira.** Kupitia Ubia Mkakati wa Alizeti: wakulima wamekuwa wakipewa msaada katika kuinua tija kwenye uzalishaji wa alizeti kwa namna ambayo inahakikisha kuwepo kwa usimamizi mahiri wa mali asili.

## Wadau muhimu kwenye Ubia Mkakati wa Zao la Alizeti

- Wizara ya Kilimo (MOA)
- Wizara ya Viwanda na Biashara (MIT)
- SNV
- TASUPA
- TANTRADE)
- AMDT
- ANSAF
- TADB
- Bytrade
- Sunflower Development Company
- MBESOPA
- Raphael Group
- CRDB
- NMB
- TCCIA
- Kituo cha Uwekezaji Tanzania
- Mamlaka ya Serikali za Mitaa
- Sekretarieti za /Mikoa/Regional Secretariats
- TRA
- Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA)
- Taasisi ya Kuhakiki Mbegu za Kilimo (TOSCI)
- Silverlands
- Dalberg
- Chuo cha Utafiti wa Kilimo (TARI)

## CHANGAMOTO NA FURSA MUHIMU

| FURSA | CHANGAMOTO |
|---|---|
| Kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu bora za Alizeti: | Uhaba wa upatikanaji wa mbegu bora za alizeti, Kiwango kidogo cha matumizi ya mbegu bora za alizeti, matumizi ya mbegu zenye uzalishaji mdogo wa alizeti, tija ndogo ya uzalishaji wa alizeti |
| Kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu za alizeti kwa ajili ya uchakataji/usindikaji | Uhaba wa mbegu za alizeti kwa ajili ya usindikaji- Upungufu wa mbegu za alizeti kwa ajili ya usindikaji, aina ya mbegu chotara iliyopo ni ghali, utunzaji duni wa mbegu za alizeti baada ya mavuno, matumizi ya teknolojia duni ya kizamani kwenye usindikaji |
| Kuongezeka kwa Upatikanaji wa huduma za kifedha na bima ya mazao | Upatikanaji mdogo wa huduma za kifedha na bima ya mazao- upatikanaji mdogo wa mikopo kwa wanaomiliki vinu vya usindikaji na wakulima wadogo, ukosefu wa bima ya mazao |
| Ubora wa bidhaa bora zitokanazo na zao la alizeti unaokidhi ushindani katika soko la Ndani na la Kimataifa | Hali duni ya bidhaa zitokanazo na zao la alizeti isiyokidhi ushindani katika Soko la Ndani na la Kimataifa- ukosefu wa vifungashio sahihi, Shirika la Viwango (TBS) kushindwa kutoa vyeti vya uhakiki kwa wasindikaji wengi |



### Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia:


SAGCOT Centre Limited

Gholofa ya 5, Jengo la Ikon
Bains Avenue, Masaki
S.L.P 80945
Dar es Salaam, Tanzania

**Simu:** +255 22 260 1024
+255 22 260 0146
**Faxi:** +255 22 260 2368

**Barua Pepe:** info@sagcot.co.tz
**Tovuti:** www.sagcot.co.tz